**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI KISANGA**

S.L.P. 21,
**MIKUMI**

15/12/2020

Kumb. Na: KSS/ADM/F.1/2021
………………………………………………
………………………………………………

YAH: **MAAGIZO YA KUJINGA NA SHULE YA SEKONDARI KISANGA WILAYA YA KILOSA MKOA WA MOROGORO**

1.0. Utangulizi

Ninayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari (kidato cha kwanza) katika shule ya sekondari Kisanga ipo katika kijiji cha Kisanga, Kata ya Kisanga, Tarafa ya Mikumi,umbali wa takribani km 100 kutoka makao makuu ya wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro **Muhula wa amsomo utaanza siku ya jumatatu tarehe 11/01/2021 saa 1:30 asubuhi.**Hivyo wanafunzi **wa hosteli waripoti siku ya jumapili tarehe 10/01/2021 saa 10:30 jioni. Kwa sababu yoyote ile,** hakuna mwanafunzi atakayepokelewa baada ya kipindi cha siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe 11/01/2021

2.0. Mambo muhimu ya kuzingatia

Mwanafunzi unahihitaji kuwa na vitu vifuatavyo ili upokelewe shuleni

2.1. Sare za shule

a) Mvulana

i) Suruali mbili za aina ya 'Kitambaa kilichoam,batanishwa' zenye mifuko mitatu ( isiyo ya kubandika).ziwe za heshima, siyo za kubana au 'modo' vinginevyo hazitakubalika. ( kitambaa kinapatikana shuleni)

ii) Mashati mawili meupe ya tetron (tomato) yenye mikono mifupi

iii) **T-shirt 1 ya bluu yenye nembo ya shule – Inapatikana shuleni kwa sh 8000/=**

iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi na vinavyofungwa kwa gidamu/kamba

b) Msichana :

i) Sketi mbili za aina na rangi ya kitambaa kilichoambatanishwa mshono aina ya linda box na uerfu usiopungua inchi 2 chini ya magoti ( Kitambaa kinapatikana shule)

ii) Mashati mawili meupe ya tetron (Tomato) yenye mikono mifupi

iii) **T-shirt 1 ya bluu yenye nembo ya shule – Inapatikana shuleni kwa Tsh 8,000/=**

iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi aina ya 'simpo za wanafunzi"

c) Wavulana na wasichana

2.2 . Tai ndefu iliyoshonwa kwa kitambaa cha rangi ya suruali/sketi ya shule

2.3. Soksi jozi mbili ziwe rangi nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana)

2.4 Sweta maalumu yenye nembo ya shule – inapatikana hapa shuleni kwa sh. 18,000/=

2.5 Vifaa vya darasani : mkebe wa Hisabati (mathematical Set), madaftari makubwa (counter books) 12, kalamu ya wino (pen) bluu/nyeusi, faili (file cover) 1, na begi (mfuko wa kubebea madaftari)

2.6 Vifaa vya usafi: Jembe lenye mpini, fyekeo au panga, ndoo ndogo 1,na ufagio wa chelewa

2.7 Mavazi ya michezo : raba, socks, jexi rangi nyeupe (kwa wasichana) na rangi ya kijani kwa wavulana)

2.8 Nembo ya kubandika kwenye mfuko mfuko wa shati ya shule – zinapatikana shuleni kwa sh 4000 kila moja.
2.9 Saa ya mkononi
2.10. Angalizo: vifaa vyote hivi ni lazima na vitahakikiwa siku ya kuripoti shuleni.atakayepungukiwa kifaa hata kimoja hatapokelewa
3.0 Wanafunzi wa Hosteli (Hostelers)
Shule inazo nafasi chache sana kwa wanafunzi ambao kwa hiari yao wenyewe nay a wazazi wao huamua kuishi shuleni (hosteli). Wanafunzi hawa hupata huduma ya kulala, chakula ( asubuhi,mchana na jioni), kujisomea muda wa ziada pamoja na malezi .Hivyo ili kumudu gharama za ununuzi wa vyakula maandalizi yake wapishi, kuni,umeme walezi (matron na patron) n.k kila mzazi wa mwanafunzi wa hosteli atachangia Tsh 600,000/= kwa mwaka. Fedha hiiyote inaweza kulipwa shuleni kwa mkupuo au kwa awamu. (Yaai January 200,000/= april 100,000/=, julai 200,000/= na sept. 100,000/=
**N;B Kiasi chochote cha fedha kilicho chini ya viwango hivi hakitapokelewa**.
Aidha , pamoja na mahitaji ya jumla kwa wanafunzi wote, mwanafunzi wa hosteli utapaswa kuja na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya matumizi binafsi

- Godoro futi $2\frac{1}{2}$ x 6
- Sanduku la chuma (Tranka ) lenye kufuli.
- Shuka mbili na blanketi 1. (shuka rangi ya blue bahari)
- Nguo za kushindia (suruali 2 au sketi rangi nyeusi, T-shirt 2 za rangi ya bluu zenye nembo)
- Tarck suit nyeusi yenye mistari myeupe pembeni
- Vyombo vya chakula: kikombe, kijiko, sahani, bakuli
- Vifaa vya usafi : ndala , (kandambili), sabuni,mswaki,dawa ya mswaki, mafuta ya kupakaa, kitana , taulo/kipande 1 cha khanga ( kwa wasichana)
- Tochi yenye betri
    - Muhimu: Maombi ya nafasi ya hosteli yafanyike kwa kuwasiliana na mkuu wa shule mapema kabla ya shule kufunguliwa. Simu ya mkuu wa shule ni 0787 232507

3.0 Utaratibu wa malipo
Malipo yote kwa ajili ya chakula yafanyike kwa mhasibu ambaye atakupatia risiti/stakabadhi. NB: Usitoe fedha yoyote kwa mtu yeyote bila kupewa risiti

4.0 Hitimisho
Nakupongeza tena kwa kuchaguliwa kwako nikiamini kuwa utatumia nafasi hii uliyopata kusoma kwa bidii na kuwa mfano wa kuigwa kwa tabia na mwenendo mzuri ili hatimaye ufikie malengo yako kwa manufaa yako na Taifa kwa ujumla.
Mwisho, nimekuwekea viambatanisho vifuatavyo

- Kiambatisho Na 1. Sheria na taratibu muhimu za shule tafadhari zisome na kuzielewa ili ziwe dira ya maisha yako ya uanafunzi hapa shuleni
- Kiambatisho Na 2 – fomu ya usajili na tamko la utii wa sheria. Fomu hii uijaze wewe mwenyewe pamoja na mazazi /mlezi wako kwa usahihi
- Kiambatisho Na 3. Medical Examination form. Unatakiwa kuipeleka kwa daktari wa kituo cha tiba kinachotambuliwa na serikali ili akupime na kukujazia fomu hii.

NB: Viambatisho Na. III. Viwasilishwe kwa mkuu wa shule siku utakaporip[oti shuleni vikiwa vimejazwa na wahusika kwa usahihi
Nakutakia maandalizi mema na karibu sana shule ya sekondari Lisanga!

STEMAN . P. KALESI
MKUU WA SHULE

THE HEADMASTER
LISANGA SEC. SCHOOL
P. O. Box 21
MIKUMI

*Kiambatisho Na I*

**OFISI YA RAIS- TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI KISANGA, S.L.P. 21, MIKUMI.**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Hivyo mwanafunzi unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
3. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)-kwa wanafunzi wa hosteli.
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
6. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
9. Kutunza mali za umma.

**Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule:**

1. Wizi.
2. Uasherati na ushoga.
3. Ubakaji.
4. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuberi, ugoro,sigara na kadhalika.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau bendera ya Taifa.
8. Kuwa mjamzito au kusababisha mimba.
9. Kuoa au kuolewa.

10.Kutoa mimba.

10.Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

11. Kukataa adhabu kwa makusudi.

12. Kuwa na **simu** ya mkononi ukiwa shuleni.

Nakutakia utekelezaji mwema

*Kiambatisho Na. II*

**OFISI YA RAIS- TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI KISANGA, S.L.P. 21, MIKUMI.**

**FOMU YA USAJILI NA TAMKO LA UTII WA SHERIA**

**SEHEMU A: Ijazwe na Mwanafunzi:**

Jina la mwanafunzi:.................................................... Jinsia (ME/KE):..............
Tarehe ya kuzaliwa:............................ Mahali pa kuzaliwa:..................................
Dini:.......................... Kabila:............................

Jina la mzazi/mlezi:....................................................

Kazi yake:.......................Namba ya simu:................................
Anuani..................................................

Nitasoma hapa shuleni nikiwa mwanafunzi wa: (*wekavema au tickpanapohusika*)

1. Kutwa (Day) ☐ 2. Hostel ☐

TAMKO: Nakiri kwamba nimesoma kwa makini sheria za shule na kuzielewa. Nimekubali na ninaahidi kuzitii kwa manufaa yangu, ya shule na umma kwa ujumla.

Saini ya mwanafunzi:................................ Tarehe:...........................

**SEHEMU B:Ijazwe na Mwalimu Mkuu wa S/Msingi alikosoma mwanafunzi:**
*Nathibitisha/ Sithibitishi kuwa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu alihitimu elimu ya msingi katika Shule ya Msingi.............................. Mwaka.............. na alifanya mtihani wa Taifa kwa Namba.................................. Aidha, kwa ninavyofahamu, tabia yake ni *nzuri/ wastani/mbaya. (*Futa isiyohusika*).

Jina la Mwl.Mkuu:..................................... Saini:........................

Tarehe:............................

Mhuri:

**SEHEMU C: Ijazwe na Mzazi/Mlezi:**
Mimi Ndugu...................................................... nakiri kwamba nimesoma kwa makini sheria za shulena maelekezo yotekama yalivyoandikwa katika barua yenye Kumb. Na: KSS/ADM/F.1/2021 ya tarehe 15/12/2018.
Nimekubali na ninaahidi kwamba nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha kuwa mwanangu (*Jina*)................................................ anafuata sheria za shule na anasoma kwa bidii. Pia nitahakikisha mwanangu anapata mahitaji yote ya shulekwa wakati. Aidha, kama mzazi/ mlezi, ninatambua kuwa elimu ni haki ya msingi ya mtoto hivyo ni wajibu wangu kuhakikisha mwanangu anahudhuria shule kila siku na kupataelimu kwa manufaa yake na Taifa kwa ujumla.

Saini................................ Mzazi/Mlezi: ...............................................

Tarehe: ...........................

*Kiambatisho Na. III*

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**KILOSA DISTRICT COUNCIL**

TO THE MEDICAL OFFICER,
Kindly examine the below named student and record the results in this form.

NAME OF STUDENT: …………………………………………………… AGE………………

A. MEDICAL HISTORY:

| | YES | NO |
|---|---|---|
| Tuberculosis | | |
| Asthma | | |
| Heart disease | | |
| Jaundice | | |
| Peptic ulcers | | |
| Epilepsy | | |
| Diabetes mellitus | | |
| Kidney problem | | |
| Anaemia | | |
| Neurosis | | |

B. PHYSICAL EXAMINATION:

Respiratory system -……………………………………………………
Cardiovascular system -……………………………………………………
Gastrointestinal system -……………………………………………………
Urinary system - ……………………………………………………
Reproductive system - ……………………………………………………
Eye: R:-……………………………………………………
L:-……………………………………………………
E.N.T- ……………………………………………………

C. INVESTIGATION:

1. Blood -HB……………………………………………………
-WBC……………………………………………………
-ESR……………………………………………………
-VDRL Test……………………………………………………
2. Urine - Pregnancy……………………………………………………
-Sed……………………………………………………
3. Stool……………………………………………………

**I have examined the above student and considered that he/she is physically and mentally fit/ unfit for further studies.**

Medical Officer's name……………………………………………………

Signature……………………………… Designation;………………………………

Station;……………………………… Date;………………………………